# LEARNING BY EAR 2009
## Economics – 6th episode

## SUCCEEDING IN THE BUSINESS WORLD

**Series**: **‘‘THE STORY OF TWO YOUNG PEOPLE, WHOSE SUCCESS STEMS FROM THEIR POCKET MONEY’’**

**Author:** **Frédéric GAKPARA**
**Editors:** **Yann Durand and Sandrine Blanchard**
**Translator:** **Anne Thomas**
**Kisuaheli:** **Eric Ponda**

**SIXTH EPISODE**: **"A loan at last!"**

**Characters**:
**John** *(18-year-old boy, twin.)*
**Jane** *(John's twin sister.)*
**Dad** *(Twins' father, 47.)*
**Driver** *(Taxi-brousse driver, 50-year-old man)*
**Shopkeeper***(Taxi-brousse passenger, 40-year-old man.)*
**Office worker** *(56-year-old man at the Chamber of Commerce.)*
**Woman behind the counter** *(Employed by Chamber of Commerce, 40ish.)*
**Narrator**

| **Learning by Ear Soundtrack** |
|---|

## Intro

**NARRATOR**: Hujambo msikilizaji wa Deustche Welle na karibu kwa makala nyingine ya Learning By Ear tukiwa bado tunazungumzia masuala ya Uchumi na Biashara. Hadithi tunayoiangazia ni ya vijna Mapacha ambao kutokana na ukakamavu wao wa kubania matumizi wamefanikiwa kuanzisha biashara. Ni mwaka mmoja sasa tangu John na Jane walipowaandikia Baba yao mdogo Sami na Fo Blam kuwaomba msaada ili wapanua biashara yao katika soko la Ulaya.Kupitia msaada huo wawili hao sasa wamefanikiwa kumpata mgawaji wa mazao ya kilimo katika soko la Ulaya ambaye anakubali kununua bidhaa zao. Kusafirisha bidhaa katika mataifa ya kigeni ni gharama. Ingawa John na Jane wameweka akiba ya kutosha , ni mkopo tu unaoweza kuwasaidia kufanikisha mpango huu. Andamana nasi kwa makala ya leo tusikie yatakayo jiri.

**Scene 1, THE JOURNEY**
JANE, DAD, DRIVER, SHOPOWNER

**ATMO**: *Sound of a taxi-brousse engine. Passengers complain and cough because of the dust.*

**NARRATOR**: Jane na Babake wakiwa katika basi la usafiri wa Umma. Wameandamana kuhudhuria mazishi umbali wa kilomita kadhaa kutoka

nyumbani. Njiani Jane anajaribu kumshawishi Babake kuwaunga mkono katika biashara yao.

**1. Jane**: Baba najua hufurahii kutuona tukifanya bishara, lakini kwa taarifa,unajua kwamba hadi sasa tumefakiniwa kupata faida ya faranga milioni 1.7?

**2. Dad**: Siwezi kukuamini. Muliwezaje kuokoa kiasi kikubwa hivyo cha pesa?

**3. Jane**: Ni kweli Baba!. Baadhi ya maduka ya Super Market sasa yamekubali kuuza njugu tunazotayarisha kutokana na ubora wake na jinsi tunavyo zipakia kwenye pakiti. Hali kadhalika unga wa Njugu Karanga tunaotayarisha umepindukia kupendwa na wengi kutokana na jinsi tunavyouhifadhi kwenye chupa, mifuko yenye nembo za kuvutia .Kwa hivyo tumefanikiwa kupanua soko letu.

**4. Dad**: (*skeptical*)
Na kuhusu mtihani wenu wa mwishoni mwa mwaka? Lini mtaachana na bishara hiyo na kuzingatia masomo yenu?

**5. Jane**: Baba unajua kuwa mimi na John hatujawahi kuanguka mtihani hata mmoja.Tunazingatia na kuchukulia masomo yetu kwa umuhimu mkubwa sana Baba. Tunafahamu kwamba tukitilia mkazo yote, hapana shaka tutafaulu mtihani.

**6. Dad**: Kwa hivyo unamaana kwamba munatarajia kufuatilia taaluma hii ya biashara maishani?

**7. Jane**: Baba mdogo Sami na Fo Blam pia wametusaidia kutafuta soko katika mataifa ya Ulaya.Baba hapa tunazungumzia kima cha mamilioni ya mapesa! Tutaweza kuwajiri zaidi ya watu 20 kutusaidia, nasi kazi yeti itakuwa wakurugenzi wasimamizi Baba. Tayari tumepiga hatua kuliko wale waliomaliza masomo yao mbele yetu na bado hadi sasa wang'ang'ana kutafuta kazi . John husimamia biashara yote na masuala ya fedha na mimi nashughulika kuitangaza na kutafuta soko jipya.Nina imani kwamba siku moja tutaweza kufungua kampuni yetu!

**8. Dad**: Lakini binti yangu kati ya biashara zote ulimwenguni, wewe na kaka yako mkaamua kufanya bishara ya kuuza Njugu.?

***9.*** **Jane**: Baba usijli, ule wakati wa kuzunguka katika barabara za mji tukibeba Njugu, umekwisha.Hivi sasa tunangalia namna nyingine ya kuuza bidhaa zinazotokana na Njugu . Tunataka kuuza bidhaa zinazotengenezwa kutokana na njugu ambazo zitapindukia kupendwa katika soko la nje. Na tayari tunapendekeza jina la Kampuni yetu ***"Appetizers of the Tropics".***

**10.** **Dad**: (*warming to the idea*)
Ni jina zuri sana ! Jane, ni furaha yangu kuwaona mkizungumzia ufanisi wa mradi wanu. Na hapana shaka hiyo huwa furaha ya kila Mzazi.Lakini mkumbuke kila jambo linawakati wake.Bado nyinyi ni wadogo sana wasi wasi ni kwamba huenda mkafadhaika maishani mkiwa bado wadogo. Mtoto anapasa kufurahia utoto wake badala ya kujiingiza mapema katika mbio hizi za uliwengu. Huo ndio wasi wasi wangu tu!.

**11.** **Jane**: Sasa naelewa wasi wasi ulionao kila wakati unapotushauri… mimi na John, Baba…!

**12.** **Dad**: Fafanua.

| | | |
|---|---|---|
| 13. | **Jane**: | Wakati mwengine pia hushikwa na wasi wasi, sio kwa sababu yangu mimi binafsi, bali kumhofia John. Nahisi nina jukumu katika kila jambo analolifanya John.Mara nyingi yeye. husema mimi najifanya kuwa kama Mamake Lakini yote tunayofanya ni kwa ajili yako Baba,..kwa heshima yako, ili kuuthiibitishia ulimwengu kwamba ulifanya kila juhudi kutulea hata baada ya mama kuiaga dunia!. |
| 14. | **Dad**: | Ninahakika mahli alipo anafurahia juhudi zenu!. |
| 15. | **ATMO**: | *Silence…* |
| 16. | **Jane**: | (*hesitating*)<br>Baba… |
| 17. | **Dad**: | Naam binti yangu ? |
| 18. | **Jane**: | Tunakuhitaji utudhamini tuweze kupewa mkopo wa benki. |
| 19. | **Dad**: | Kwanini mnataka niwe mdhamini wenu, nyote mumetimiza umri wa miaka 18!. |
| 20. | **Jane**: | Benki inasema kuwa hata ukiwa na umri wa miaka 60 unahitaji mdhamini ndio uweze |

kupewa mkopo.Mbali na hayo uwe na akiba ya kutosha kugharimia mkopo huo, na tatu, akaunti yako iwe na akiba ya theluthi moja ya mkopo unaotaka kuchukua. Lakini kwa mtu anayetaka kuchukua mkopo zaidi ya laki tano, anahitajika kuwa na dhamana ya nyumba.

**21. Dad**: Kwanini sheria nyingi hivyo? Wanataka kusaidia watu au ni porojo tu?

**22. Jane**: Hiyo ndio sababu tumejikokota kwa muda wa mwaka mmoja sasa.

**23. Driver**: (*In bad English*)
“ Mwanamke anayetaka kuteremka Tinwango lipa nauli yako sasa ..

**24. Dad**: Na mnataka kuchukua mkopo kiasi gani ?

**25. Jane**: Milioni nne elfu mia tano…

**26. Dad**: Ngapi ? Mkopo mkubwa hivyo mtaulipa vipi?

**27. Jane**: Tumepata kandarasi ya milioni saba. John amefanya hesabu gharama zote, kununua Njugu, mifuko,kukodisha mashini,usafirishaji, gharama zote ni faranga milioni tatu elfu mia

tano. Na tuweke akiba ya milioni moja ya kwa hali yoyote ya dharura inapotokezea.

**28. Shopkeeper**: Dereva Dereva ! Unanipitisha kwenda wapi? Mimi huteremka hapa wakati wote, au unasahau ?

**29. . Driver**: (*Bad English again*)
"Sasa nitajuaje? Kwani mimi nasoma akili ya kila mmoja hapa??"

**30. ATMO**: *The taxi stops, the customer gets out and the car starts up again.*

**31. Dad**: Sasa mnauhakika gani mutaweza kulipa mkopo huo?

**32. Jane**: Kandarasi tulizopata zinatosha.Baba mdogo Sami anatuwakilisha nchini Switzerland na Fo Blam anatuwakilisha nchini Ujerumani.Wote wanatuunga mkono!.

**33. Dad**: Nitawasiliana nao ili nipate ufafanuzi zaidi.Iwapo biashara yenu ni nzuri na yenye matumaini,hapana shaka nitawasaidia. Kwa hivyo musemavyo ni kwamba tayari mna akiba ya theluthi moja ya mkopo munaotaka

kuchukua.Pongezi! Nitawadhamini na pia kwa dhamana ya nyumba ikiwezekana.

**34. Jane**: (*Hugs her father*)
Asante sana Baba, nilijua tu utatusaidia!

**35. Dad**: Lakini ni lazima mutafute mdhamini wa pili.

**36. Jane**: Tayari tumempata, Bibi alimuomba Da Aleye atudhamini na akakubali.Sasa ni wewe uliyesalia Baba!.

**37. ATMO**: *The taxi-brousse comes to a stop.*

**38. Dad**: Sasa nimekubali. Lakini tafadhalini msichukulie uamuzi huu kuwa wa moja kwa moja, ni lazima ni chunguze ombi lenu kwa makini tutakaporejea nyumbani , sawa ?

**39. Jane**: Sawa Baba.

**40. Driver**: *(In bad English again*)
“ Mtu nalala vibaya na gari nakuja ?”

**NARRATOR**: Kwa upande mwengine, John amekuwa aking’ang’ana kupata cheti cha kuendesha shughuli zake za kiuchumi.Na hatimaye

anafanikiwa kujisajili na chama cha wanabiashara na viwanda.

**Scene 2, AT THE CHAMBER OF COMMERCE**
JOHN, OFFICE WORKER, THE WOMAN BEHIND THE COUNTER…

**41.** **Office worker**: Ndio, rafiki ?

**42.** **John**: Nilikuja jana kupata maelezo ya kuwa mwanachama na kupata cheti kuhusu masuala ya Uchumi. Ndio sababu leo nimerudi kujaza fomu.

**43.** **Office worker**: Na yuko wapi mhitaji?

**44.** **John**: Ni mimi!.

**45.** **Office worker**: (*Very surprised*)
Eti ? Hebu nipe kitambulisho (*a pause*)
Lakini wewe bado ni mwanafunzi !

**46.** **John**: Lakini nasimamia bishara yangu mwenyewe!.

**47.** **Office worker**: Unaweza kuthibitisha?

**48.** **John**: Kwani siku hizi kuna cheti kinachotolewa kwa wachuuzi wa barabarani humu nchini?

**49. Office worker**: Ohh, sasa kwa kuwa umetimu umri wa 18 unaona una haki ya kuongea ujeuri mbele yangu!

**50. John**: Nimekuja hapa kupataa kadi ya uanachama sio kubishana na wewe!.

**51. Office worker**: (*Very annoyed*)
Picha mbili! Kitambulisho cha taifa! Nenda ukalipe faranga elfu 140 kisha ujaze hizi fomu hizi!

**52. ATMO**: *Office worker practically hits the table when he gives John the forms. John picks them up and his steps can be heard as he makes his way to the counter.*

**53. John**: (*To himself*)
Sijui kwanini watu wanakosa utu namna hii! Kwani anataka ni muhonge?
(*To the woman behind the counter)*
Habari ,Mama!

**54. Woman behind the counter:**
Nzuri ! ehhe?

**55. John**: Ningependa kulipia kadi ya uanachama wa masuala ya Uchumi.

**56. Woman behind the counter**:

Lete elfu 140!

**57. ATMO**: *We hear John counting the notes. The woman takes the money. Keyboard sounds.*

**58. Woman behind the counter**:

Jaza hizi fomu tafadhali ,na uniachie kopi na kopi nyingine umpelekee afisa wa kwanza pamoja na hii risiti. Unaitwa nani ili tufanya haraka?

**59. John**: John MIBLEMI.

**60. The woman behind the counter**:

Unamiliki kampuni ?

**61. John**: Ndio ! Inaitwa ***"Appetizers of the Tropics".*** Ni kampuni ya biashara. Nimemaliza kujaza hizi fomu Mama.

**62. The woman behind the counter**:

Nipe !

(*Mumbling)*

Sawa… hapa … sawa… vizuri hapa… Pia nahitaji sahihi ya pili hapa.

**63. John**: Oh, kweli pole! (*A pause*) Sawa sasa ndio hizi!

**64. Woman behind the counter**:
Sawa kabia ! Hii hapa risiti yako!Kila la kheri katika biashara yako!

**65. John**: Asante sana Mama!

**66. ATMO**: *We hear John's steps as he goes back to the office worker.*

**67. John**: Nimekamilisha !

**68. Office worker**: Weka sahihi katika daftari hili!

**69. John**: Sawa.

**70. Office worker**: Sawa hii ni kadi yako na kitambulisho !

**71. ATMO**: *John's steps again as he exits.*

**72. John**: (*murmuring*)
Heshima kidogo tu haiwezi kukudhuru au sivyo!

## Outro

**NARRATOR:** Katika muda wa siku chache shughuli zinazidi kuwa nyingi kwa wafanyi bishara hawa mapacha. Baba yao hatimaye amekubali kuwadhamini kupata mkopo wa Benki. John na Jane wanafahamu fika kibarua kilicho mbele yao.

**73. Closing soundtrack to be left running after the outro and brought up**

**NARRATOR:** Wana imani kuwa watafaulu, Lakini je watatimiza ndoto hiyo? Kwa mengi zaidi ungana nasi wakati ujao kwa kipindi kingine cha kusisimua. Na kumbuka ukipenda kukisikiliza tena kipindi hiki au ukiwa na maoni tembelea mtandao wetu wa **dw-world.de/l b e**
Hadi wakati huo basi kwaheri kwa sasa!

**Music up**

END